*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: **ISSN 2523-6725** (online)
**October 2024 Vol. 8, No. 10**
**Citation:** Kimwe, P & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Za Maisha Katika Tamthilia Za Kiswahili: Uchunguzi Wa *Bembea Ya Maisha* Na *Mstahiki Meya*. *Journal of African Interdisciplinary Studies*, 8(10), 199 – 214.

# Usawiri Wa Changamoto Za Maisha Katika Tamthilia Za Kiswahili: Uchunguzi Wa *Bembea Ya Maisha* Na *Mstahiki Meya*

[1]Purity Kimwe and [2]Joseph Kariuki Gakuo

[1]Purity Kimwe, Chuo Kikuu cha Mount Kenya
Corresponding author email address: puritykimwe86@gmail.com
[2]Joseph Kariuki Gakuo mhadhiri mwandamizi, Chuo Kikuu Kishirikishi cha Bomet

**Ikisiri**
Suala la changamoto za maisha ni suala nyeti katika jamii kwa kuwa binadamu wanakumbwa na changamoto mbalimbali kila uchao. Siku baada ya siku binadamu yumo mbioni kujaribu kuzitatua na kila uchao kunaibuka changamoto tofauti tofauti ambazo zinaonekana kutishia maisha yake, hivyo basi inambidi kujikakamau ili aweze kuendeleza maisha yake. Wanajamii hawawezi kuwa wanaelewa kila kitu kutokana na utambuzi wa tajriba zao. Kuna mambo mapya yanayoibuka kila uchao katika jamii mengine yakiwa ni yale ya kawaida ila yenye kuchukuwa mikondo mipya. Utafiti huu ulikusudia kuchunguza suala la changamoto za maisha katika tamthilia za Kiswahili kwa kurejelea tamthilia za *Bembea ya Maisha* (Arege 2022) na *Mstahiki Meya* (Arege 2009) zilizoandikwa na Timothy Arege. Utafiti huu ulinuia kuangazia changamoto zinazokumba jamii pamoja na athari zake kwa mujibu wa tamthilia teule. Utafiti huu ulijikita katika mtazamo wa nadharia ya uchanganuzi nafsia na ule wa nadharia ya uhalisia. Mihimili ya nadharia hizi ilitumika ili kuongoza utafiti huu kuafiki malengo yake. Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo; Kuainisha changamoto za maisha namna zilivyosawiriwa katika tamthilia zilizoteuliwa, kuchunguza athari za changamoto hizi jinsi zilivyosawiriwa katika tamthilia hizi na kutathmini mbinu za kukabiliana na changamoto hizi katika jamii jinsi zinavyopendekezwa na mwandishi katika tamthilia teule. Utafiti ulifanyika maktabani ambako tuliangalia makala yaliyoandikwa kuhusu tamthilia, tasnifu zilizoandikwa kuhusu tamthilia kwa jumla na pia zilizoandikwa kuhusu masuala ibuka. Pia tulirejelea majarida, vitabu na magazeti yaliyoandikwa kuhusu masuala ibuka. Utafiti huu ulitumikiza sampuli ya kusudio katika kuteua tamthilia hizi za utafiti ambazo zilisomwa kwa kina ili kupata data ya kuchanganuliwa. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo na ufafanuzi. Inatarajiwa kuwa matokeo ya utafiti huu yatawasaidia wanajamii kukabiliana na hali halisi maishani na pia kufungua uwanja huu kwa tafiti za baadaye kuhusu masuala ibuka katika jamii. Matokeo ya utafiti huu pia yanatarajiwa kufanikisha kueleweka kwa kazi hizi zenye ujumi wa kipekee zilizoandikwa na kutungwa na mwandishi na mwalimu tajika Kenya.

*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: ISSN 2523-6725 (online)
October 2024 Vol. 8, No. 10
**Citation:** Kimwe, P & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Za Maisha Katika Tamthilia Za Kiswahili: Uchunguzi Wa *Bembea Ya Maisha* Na *Mstahiki Meya*. *Journal of African Interdisciplinary Studies*, 8(10), 199 – 214.

**Maelezo ya istilahi muhimu**

**Fasihi**

Ni sanaa inayotumia lugha kwa ubunifu ili kuwasilisha masuala kuhusu binadamu, maisha yake na mazingira anamoishi

**Fasihi andishi**

Ni aina ya fasihi inayohifadhiwa katika maandishi na hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya maandishi.

**Tamthlia**

Ni utanzu wa fasihi andishi. Ni Kitabu cha mchezo wa kuigiza. Tamthilia inaweza kuigizwa jukwaani mbele ya hadhira hai.

**Bembea**

Ni kifaa cha kujining'iniza kinachotengenezwa kwa kamba, nyororo au waya na kumwezesha mtu kustarehesha juu yake kwa kwenda mbele na nyuma, juu na chini.

**Bembea ya Maisha**

Ni kule kupanda na kushuka, taabu na raha za maisha. Ni tamthlia teule ya uatafiti wetu

**Masuala ibuka**

Haya ni mambo mapya ambayo yanaikumba jamii ya sasa inayopitia mabadiliko mengi.
Maudhui ambayo yanazungumzia mambo ambayo yametokea katika eneo ambalo watu wanaishi
na ambayo yana athari kubwa kwa watu wanaoishi huko.

**Usawiri:**

Ni kuumba wahusika, kuchora vitu au jambo akilini mwa anayesoma kazi ya fasihi. Kitendo cha
kumpa mhusika au wahusika sifa katika kazi ya fasihi.

**Wahusika:**

Viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ili wawe wasemaji wakekatika kuufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa

*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: **ISSN 2523-6725** (online)
**October 2024 Vol. 8, No. 10**
**Citation:** Kimwe, P & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Za Maisha Katika Tamthilia Za Kiswahili: Uchunguzi Wa *Bembea Ya Maisha* Na *Mstahiki Meya*. *Journal of African Interdisciplinary Studies*, 8(10), 199 – 214.

**Usawiri Wa Changamoto Za Maisha Katika Tamthilia Za Kiswahili: Uchunguzi Wa *Bembea Ya Maisha* Na *Mstahiki Meya***

[1]Purity Kimwe and [2]Joseph Kariuki Gakuo

## Utangulizi

Mada hii iliteuliwa kwa sababu kadha. Ingawa kuna waandishi wengi wa tamthilia, ni tamthilia chache za hivi punde zinazoshughulikia masuala ibuka katika jamii. Mada hii kwa hivyo ni muhimu sana katika kuziba pengo la uchunguzi wa suala ibuka la changamoto za maisha kama lilivyosawiriwa katika fasihi andishi hususan tamthilia za Kiswahili: *Bembea ya Maisha* (Arege: 2022) na *Mstahiki Meya* (Arege:2009) Mintarafu ya hili, inaakisi migongano ya kitamaduni, uhalisia wa mambo na matamanio ya wahusika binafsi. Kuna vuta-nikuvute zinazotishia familia katika jamii ya leo pamwe na masuala ya kijumla ya ndoa na uhusiano wa kijamii. Kuna tafiti chache mno ambazo zimefanywa kuhusu usawiri wa masuala ibuka katika jamii. Hasa kadri ajuavyo mtafiti, hamna utafiti kama huu uliowahi kufanywa kuhusu tamthilia ya Kiswahili. Hivyo kuna haja kulitafitia ili kuziba pengo hili.

Utafiti huu ulikusudia kuonyesha kuwa fasihi hususan tamthilia ya Kiswahili, ina dhima muhimu ya kuangazia masuala ibuka katika jamii. Hili linaifanya tamthilia kuchukuliwa kuwa na umuhimu zaidi ya burudani. *Bembea ya maisha* (Arege: 2022) na *Mstahiki Meya* (Arege: 2009) zinaibua masuala kadha nyeti na yafaayo kuangaziwa katika maendeleo ya jamii. Mtunzi kwa mfano, anasawiri suala ibuka muhimu kuhusu changamoto zinazowakumba watoto, wawe wa kike au kiume katika ndoa. Isitoshe, anaangazia kuhusu umuhimu wa kuwaelimisha watoto hasa wa kike, vita vya kinyumbani baina ya wazazi vinavyoweza kuwaathiri wanao kimaisha na madhila ya wanawake yanayotokana na ndoa miongoni mwa mengine.

## Uhakiki wa fasihi kuhusu mada

Karanja (2008), kwa upande wake alijihusisha na Usawiri wa masuala ibuka katika fasihi ya watoto. Utafiti huu ulijadili usawiri wa maswala-ibuka katika hadithi za watoto. Ulikusudia kuainisha masuala ibuka katika vitabu teule vya fasihi ya watoto, kuonyesha mitindo iliyotumiwa kusawiri masuala haya na kuchunguza ufaafu wa mitindo hiyo kwenye fasihi ya watoto. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa watunzi wa fasihi ya watoto wameweza kuangazia masuala-ibuka kwenye fasihi ya watoto hivyo, watafiti wengine hawana budi ila kuangalia masuala haya katika vipengele vingine vya fasihi kama vile tamthilia. Tofauti na utafiti wetu, sisi tuliangazia fasihi andishi ya Kiswahili kwenye utanzu wa Tamthilia.

Okwena (2013) alishughulikia matumizi ya jazanda katika tamthilia tatu teule za Arege: *Kijiba cha Moyo* (2009) *Mstahiki Meya* (2009) na *Chamchela* (2007). Katika utafiti wake alichunguza aina tofauti tofauti za jazanda zilizotumiwa na watunzi katika kuwasilisha maudhui. Utafiti huu wake ulitusaidia katika kuelewa suala la changamoto za maisha ambazo ni mojawapo ya masuala makuu kwenye tamthilia zetu zilizoteule.

Fridah (2017), alishughulikia Uhakiki wa Mtindo katika Tamthilia za Arege*: Kijiba cha Moyo* (2009), *Mstahiki Meya* (2009) na *Chamchela* (2007. Utafiti huu wake ulitusaidia kumwelewa mwandishi Timothy Arege zaidi. Utafiti wa Fridah ni tofauti na huu hivi kwamba, huu ulichunguza suala la changamoto za maisha katika tamthilia za *Bembea ya Maisha* (2022) na *Mstahiki Meya* (2009) lakini yeye alitafitia mtindo katika tamthilia za mwandishi Timothy Arege.

Syekei (2017), alitafiti kuhusu nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthilia teule za kiswahili; *Kilio cha Haki* (Mazrui:1981), *Sudana* (Mazrui na Njogu:2006), *Posa za Bikisiwa* (Mohamed na King'ei:2008), na Pango (Wamitila:2003) Utafiti huu ulitusaidia katika kufahamu zaidi kuhusu tamthilia kwa jumla katika utafiti. Utafiti wake na huu wetu ni tofauti kwa sababu, yeye alichunguza maudhui ya nafasi ya mwanamke katika uongozi ila sisi tulishughulikia suala la changamoto za maisha katika tamthilia za Kiswahili.

Naye Sinzore (2019), ameshughulikia Taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka 2000 hadi 2016. Utafiti huu ulimwangazia mwanamke kwa jumla bila kuangalia masuala yake mengine sawa na tafiti zingine zilizouzingatia usawiri hasi wa mwanamke. Usawiri huu uliangazia hadhi duni ambayo mwanamke alikuwa amepewa katika jamii. Kulikuwa na wanawake viongozi kabla ya mwaka 2000 lakini hadhi yao ilikuwa chini. Hata hivyo, baadaye kulitokea mabadiliko katika jamii kuanzia mwaka wa 2000 yakapandisha hadhi ya mwanamke. Jamii ilianza kumpa mwanamke nafasi za uongozi na kumsawiri kwa njia chanya. Utafiti huu ulinuia kuchunguza iwapo usawiri wa uongozi wa mwanamke katika tamthilia ya Kiswahili uliendelea kumsawiri kwa njia hasi au umebadilika baada ya hadhi ya mwanamke kuimarika. Utafiti huu kuhusu mwanamke kiongozi ulitufaa kwa sababu suala la uongozi wa mwanamke limeanza kukita mizizi katika jamii. Hadhi ya mwanamke inaendelea kuimarika na hivyo ni wazi kwamba suala hili linafaa kuchunguzwa kwa kina. Uongozi wa mwanamke ni mojawapo ya masuala ibuka katika jamii.

Mwangi (2022) alitafitia tamthilia ya Kiswahili. Alishughulikia Changamoto Zinazowakumba Vijana katika Tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* iliyoandikwa na S. A. Mohamed (2000), na kutambua mbinu wanazotumia kusuluhisha changamoto hizi. Vijana katika jamii wana msukumo wa kuleta mabadiliko na wamekuwa kwenye mstari wa mbele kupigania haki zao na kutafuta suluhu kwa changamoto zinazowakumba. Utafiti huu ulitufaa kwa sababu baadhi ya changamoto za vijana kama vile msongo wa mawazo ni baadhi ya masuala ibuka katika jamii. Utafiti huu ulilenga kuangazia vijana ambao ni kundi moja tu katika jamii, hivyo kuna pengo la changamoto zinazowaathiri wanajamii kwa jumla.

## Methodolojia

### Eneo la utafiti

Utafiti huu ulijikita maktabani ambako kazi zote zinazohusiana na mada ya utafiti; suala la changamoto za maisha zilisomwa na kuhakikiwa. Vitabu, machapisho na makala mbalimbali kwenye intaneti yalisomwa ili kufanikisha uelewa wa mada hii. Mtafiti pia alisoma tasnifu za watafiti wengine zinazohusiana na mada hii ili kuupa utafiti wetu mwelekeo.

Eneo la utafiti huu ni fasihi andishi, katika utanzu wa tamthilia. Mtafiti ameteua tamthilia mbili za Kiswahili; Bembea ya Maisha (Arege:2022) na Mstahiki Meya (Arege:2009) ili kuangazia usawiri wa suala la changamoto za maisha katika tamthilia ya Kiswahili. Tamthilia teule zimechapishwa katika kipindi cha hivi karibuni na zinaendana na malengo ya utafiti huu.

### Idadi lengwa ya utafiti

Utafiti huu ulilenga kutumia tamthilia mbili za hivi punde; Bembea ya Maisha (Arege:2022) na Mstahiki Meya (Arege:2009). Mtafiti amelenga tamthilia hizi mbili kwa sababu zimechapishwa hivi karibuni na hivyo zinaweza kutoa picha halisi ya mambo kama yalivyo katika jamii. Tamthilia hizi pia zimetahiniwa hivi karibuni katika shule za sekondari nchini Kenya.

**Uteuzi wa sampuli**

Utafiti huu ulitumikiza sampuli ya kusudio yaani tamthilia za hivi punde za Kiswahili. Vitabu vya tamthilia vilivyochapishwa ni vingi mno na hatuwezi kuvihakiki vyote kwa undani. Katika
kushughulikia mada hii tamthilia ya Bembea ya Maisha (Arege:2022) na ya Mstahiki Meya (Arege:2009) zimeteuliwa kwa sababu zimechapishwa hivi punde. Baada ya kuzipitia tamthilia hizi kwa kina, ilionekana kuwa zingemfaa mtafiti katika kupata data muhimu ilikayomsaidia kuyajibu maswali ya utafiti. Tamthilia hizi pia zimeteuliwa kwa sababu ni baadhi ya vitabu ambavyo vimeteuliwa na kupitishwa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (K.I.C.D.) kusomwa katika shule za upili na na wanafunzi kutahiniwa katika kidato cha nne. Baadhi ya matokeo ya uchunguzi wa utafiti huu yatachangia ubora wa kueleweka kwa kazi hii pamoja na kuboresha ufunzaji kote nchini.

**Mbinu za ukusanyaji data**

Njia tofauti tofauti zilitumiwa kukusanya data katika utafiti huu. Njia hizi ni kama vile; usomaji wa kina na makini na uchanganuzi wa matini mbalimbali.

**Usomaji makini**

Utafiti huu ulikuwa na data ya kimsingi ambayo ni tamthilia za Bembea ya Maisha (Arege 2022) na Mstahiki Meya (Arege 2009). Data ya utafiti huu ilitokana na usomaji wa kina wa tamthilia hizi maktabani na kuzihakiki kwa kuongozwa na malengo ya utafiti. Hii ni kwa sababu tamthilia sawa na tanzu zingine za fasihi ya Kiswahili, inajisimamia yenyewe. Mtafiti pia alisoma Makala na machapisho ya kijumla kuhusu tamthlia ya Kiswahili.

**Uchanganuzi wa matini**

Mtafiti alihakiki tamthilia za Bembea ya Maisha (Arege:2022) na Mstahiki Meya (Arege:2009) ili kupata data ya kuchanganua. Maktabani vilevile, mtafiti alisoma makala, vitabu, majarida, machapisho na tasnifu zinazogusia masuala ya utafiti ikiwa ni pamoja na nadharia za utafiti na tafiti kuhusu tamthilia ya Kiswahili kwa jumla.

**Vifaa vya ukusanyaji data**

Mtafiti aliweza kutumia madaftari, tarakilishi, rununu, kalamu na karatasi katika kukusanya na kuchambua data. Vifaa hivi vilitumiwa ili kurekodi yaliyosomwa kutoka kwa matini yaliyopitiwa. Data iliyopatikana ilihifadhiwa kwenye tarakilishi.

**Muhtasari wa tamthilia ya *Bembea ya Maisha***

Tamthilia ya *Bembea ya Maisha* iliandikwa na Timothy Arege na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 2022. Tamthilia hii imegawanyika kwenye sehemu nne na maonyesho kumi na manne kwenye kurasa sabini na nne. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI, neno 'bembea' lina maana ya kifaa kama vile mbao, chuma au kamba kinachoning'inizwa haswa mitini kwa ajili ya kutumiwa na watu na haswa watoto kuchezea.

Ili mchezo wa bembea kuwa na mvuto, huwa kuna yule anayesukuma mwingine juu, chini, mbele na nyuma ili anayecheza afurahishwe na mchezo. 'Bembea ya Maisha' ambayo ndiyo anwani ya tamthilia hii humaanisha namna binadamu huchezeshwa na maisha siku baada ya siku. Kuna siku za furaha na zingine za huzuni na hali hizo mbili ndizo hukamilisha maisha ya mwanadamu. Kwa vile fasihi daima huwa kioo cha jamii, mwandishi wa tamthilia hii ametumia wahusika ambao wanawakilisha binadamu halisia ili kuweka wazi namna

binadamu huyu anavyozungushwa na maisha siku baada ya siku namna bembea huzungusha anayecheza nayo.

Tamthila hii ya *Bembea ya Maisha* imejikita kwa mapana kwa familia ya Yona na mkewe Sara pamoja na watoto wao Neema, Asna na Salome. Kwa vipindi tofauti kuna maisha ya furaha kwa familia hii na kipindi kingine maisha yanabadilika na kuwa ya huzuni.

Yona alikuwa mwalimu katika ujana wake ila bembea ya maisha ikamfanya kuwa mlevi tajika jambo ambalo linamfanya aachishwe kazi na kutaabika ambapo anazamia ulevi kama suluhisho la hali yake. Mwanzoni mwa ndoa ya Yona na Sara, maisha yalikuwa murua lakini migogoro iliyozuka baada ya Yona kuachishwa kazi ikamfanya Sara kupatwa na maradhi ya moyo na hivyo maisha yao kujawa na utengano wasioaulalia wala kuuamkia huku Sara akisaka matibabu mjini naye Yona akibaki mashambani. Maisha ya Sara yaliyokuwa shwari yanabadilika na kumkatisha tamaa kiasi cha kuona afadhali kufa kuliko kuishi kwa maisha ya dhiki. Mwili wake uliokuwa wenye siha unabadilishwa na maradhi na kubakia kifyefye tu.

Hata hivyo, tamthilia hii inatoa picha ya jinsi hali ya maisha ya kale ya mwafrika yanavyobadilika kila uchao kwani inamkweza mwanamke kinyume na matarajio na utamaduni wa jamii. Yona na Sara wamejaliwa watoto wa tatu wa kike; Neema, Asna na Salome na ambao wamesoma hadi kuwa wa msaada kwa familia ya wazazi wao kinyume na ilivyoakisiwa na jamii walimotoka. Mwanzoni, wanajamii na hata marafiki wa Yona waliona familia ya Yona na Sara kutokamilika bila kuwa na mtoto wa kiume lakini baadaye wale mabinti wa Yona na Sara wakawapiku watoto wa kiume kijijini kiasi cha wanakijiji kuwa na mtazamo mpya kuhusu jinsia.

Ingawa maudhui makuu yaliyopo kwenye tamthilia hii ni nafasi ya mwanamke katika jamii ya kisasa pamoja na yale ya mabadiliko, kuna maudhui mengine kama vile; ndoa, ulevi, teknolojia na maendeleo, malezi, taasubi ya kiume, utamaduni, elimu na migogoro miongoni mwa maudhui mengine. Ingawa familia ya Yona imekubwa na migogoro chungu nzima, mwishowe anajiona kuwa mkosaji kwa kuzamia ulevi huku akipuuza familia yake. Anaomba msamaha na kuwasihi mke na watoto wake kumpa nafasi nyingine kuanza na kutengeneza maisha yake upya.

**Muhtasari wa tamthilia ya *Mstahiki Meya***

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* iliandikwa na Timothy Arege na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 2009 na Kampuni ya uchapishaji ya Vide-Muwa. Tamthilia hii imegawanyika kwenye sehemu nne na maonyesho kumi na mawili yaliyojazwa kwenye kurasa sabini na saba. Tamthilia hii kama ilivyo vitabu vya fasihi vinavyochora taswira ya jamii halisia ya mwanadamu, inatoa picha ya jinsi jamii ilivyo kwa sasa.

Ni tamthilia inayotoa picha kamili ya uhusiano uliopo kati ya viongozi wa kisiasa na raia ambao haswa ndio waliowapa viongozi hawa nafasi ya uongozi. Uongozi huu licha ya kuwa na nafasi murua ya kuongoza raia kwenye upeo wa maendeleo, unawanyanyasa na kujinufaisha wenyewe.

Tamthilia inaangazia Baraza la Cheneo linaloongozwa na Meya Sosi, madiwani waliochanguliwa na wapiga kura, mazingira ya hospitalini, ofisini, kwenye viwanja vya ndege na nyumbani yote yakiwakilisha mazingira halisi ya jamii halisia. Kuna wafanyikazi na viongozi wao walio kwenye mstari wa kwanza kuteta kuhusu mazingira ya kazini yanayosinya jambo linalowafanya wafanyikazi mbalimbali kuwa na migomo na maandamano ya mara kwa mara.

Mwandishi wa tamthilia hii anaangazia matatizo ya baraza hili kama vile njaa, ukosefu wa bidhaa za kimsingi zikiwemo dawa, ahadi za uwongo kutoka kwa viongozi, ufisadi, wizi wa mali ya umma na unafiki wa kidini miongoni mwa masuala mengine nyeti. Licha ya vilio vya wafanyikazi wanaoongozwa na wahusika kama vile Daktari Siki, Tatu, Medi na Beka kupeleleka vilio vyao kwa Meya Sosi, kiongozi huyu anaonekana kutojalishwa na hali ngumu inayopitiwa na wafanyikazi pamoja na raia wa kawaida.

Watu kadhaa wanakufa kwa njaa lakini hili halimpi kiongozi wa baraza hili Mstahiki Meya kiwewe kwa namna yoyote. Kwa sababu ya huduma duni za elimu na matibabu, Meya anawapeleka watoto wake kusomea Ng'ambo pamoja na mke wake kujifungulia kule ili mtoto atakayezaliwa apate uraia wa kule. Ingawa maudhui makuu kwenye tamthilia hii ni uongozi mbaya, dhuluma na ufisadi, bado kuna maudhui madogo madogo kama vile dhihaka, migomo, unafiki wa kidini, utamaushi, magonjwa na kutowajibika miongoni mwa maudhui mengine.

Kwa vile hakuna lisilo na mwisho duniani, mwishoni mwa tamthilia kiongozi mkuu Mstahiki Meya pamoja na washauri wake wakuu Diwani I na II wanakamatwa kwa lengo la kupelekwa kizimbani ili kuelezea zaidi kuhusu mambo yanayotatiza raia wa Baraza la Cheneo. Hii ni dhihirisho kuwa hata mwovu na uovu ukikithiri kwa muda gani, baadaye una kikomo chake.

## Usawiri wa changamoto za maisha katika tamthilia za Bembea ya Maisha na Mstahiki Meya

### Umasikini

Umasikini ni hali ya ukosefu wa mahitaji ya kimsingi ya binadamu kama vile chakula, maji safi, huduma za afya, mavazi na makao kwa jumla. Umasikini unaweza kutokea kwa sababu ya makosa ya mwanadamu mwenyewe au hali za kimaumbile kama vile maradhi sugu au ukame. Umasikini unapotokea katika jamii yoyote ile, waathiriwa huhangaika huku na kule kwa ajili ya kujinasua kutoka kwa hali ile kwani huwa yenye aibu kwa waathiriwa.

Ukosefu wa mahitaji ya kimsingi unaweza kuzaa hali zingine kama vile wizi na uozo pale mwathiriwa anapojaribu kujinasua kutoka kwa hali inayomkabili. Jamii ya mwanadamu wa sasa imejawa na hali ya umasikini hapa na pale jambo ambalo linafanya waandishi wa kazi za fasihi kuweka masuala haya wazi kwa ajili ya kuchochea taasisi zinazoshughulika na mbinu za kukabiliana nayo kujizatiti ili kujenga upya heshima anayostahiki kiumbe aliye hai. Timothy Arege kwenye vitabu vyake vya *Bembea ya Maisha* na *Mstahiki Meya* ameangazia suala la umasikini katika jamii ya mwanadamu kama inavyojitokeza kwenye mjadali ufuatao; Katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*, umasikini unadhihirika pale nyumbani kwa Asna ambapo chumba ni kidogo, kitanda ndicho hutumiwa kama kiti kwani kiti cha pekee kwenye chumba kile ni kigoda tu. Vivyo hivyo, meza na jiko la gesi ni ndogo.

Kuna ishara ya umasikini pia kwani baada ya nguvu za umeme kupotea labda kwa kukosa kulipiwa, mwangaza wa taa ya chemni ni hafifu. Hii ina maana kuwa Asna hana uwezo wa kununua bidhaa za maana za chumba chake na pia hana uwezo wa kukodisha nyumba kubwa. Hali hii ya umaskini inadhihirika kwenye dondoo ifuatayo ;
*'Chumba ni kidogo na nadhifu. Kwenye upembe mmoja mna kitanda ambacho pia hutumika kama kiti. Kuna jiko ndogo la gesi, taa ya chemni ina mwangaza hafifu na nguvu za umeme zimepotea'*uk 31). Kwenye tamthilia ya *Mstahiki Meya*, hali ya umasikini unadhihirika kwenye maneno ya Waridi anapodai kuwa nchi yao ni maskini na ombaomba…

> Wazungu wanatuhimiza tuwe na mfumo wa kugawana gharama, tutafanya nini nayo nchi yetu ni maskini tu (uk 3).

Pia hali ya umasikini inajitokeza pale ambapo Mama anaulizwa na Daktari Siki kuhusu chakula alichompa mtoto ambapo anadai kuwa alimpa wali na maharangwe yaliyolala. Hili linadhihirisha kuwa hakuwa na uwezo wa kumpa mtoto wake kiamsha kinywa cha maana. ‘ ‘ *Nilimpa mtoto marangwe yaliyolala…sikuyala mimi kwa vile yalikuwa machache tu’’ (*uk 4) Pia kwenye tamthilia hii, Siki anamwambia Meya kuwa watu wanakula mizizi na matunda ya mwituni. Hii ni ishara ya umasikini kwani watu hawa hawawezi kumudu chakula cha maana. Siki anasema maneno haya kumwelezea Meya Sosi kudhihirisha umaskini uliopo miongoni mwa wanacheneo ;

> Kuna mengi ambayo hayajanyooka na hanakuhitaji uyanyooshe…watu wanakufa kila siku kwa kula mizizi na matunda ya mwituni (uk 12).

Kulingana na utafiti uliofanywa, ni wazi kuwa jamii ya mwanadamu imekumbwa na changamoto za umasikini unaojiengemeza kwenye vitengo tofauti vikiwemo ukosefu wa makao yenye heshima na ukosefu wa chakula bora miongoni mwa vipengele vingine.

**Magonjwa**

Magonjwa ni hali ya mvurugo katika utendaji wa kawaida wa shughuli za mwili na roho inayoathiri pakubwa ustawi na starehe kwa kiumbe aliye na uhai. Mwili wa kiumbe yeyote yule unapoathiriwa na magonjwa hudhoofika kiasi cha kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo na hili hutia kiumbe huyu wasiwasi wa moyo kiasi cha kuharakisha kifo chake.

Miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la magonjwa sugu na ambayo yamekuwa na ugumu wa kutibika jambo ambalo linazidi kutishia ulimwengu anamoishi binadamu. Kwa vile tunaishi kwenye karne ya wasomi, waandishi wengi wamekuwa wakiweka masuala ya magonjwa kwenye maandishi ili yasomwe na wasomi wa viwango tofauti. Waandishi wa fasihi chipukizi na waliobombea hawajaachwa nyuma katika uandishi wao kuhusu magonjwa. Wameyamwaga haya kwenye kazi zao za fasihi zikiwemo riwaya, tamthilia na hadithi fupi ambapo masuala ya magonjwa yanajadiliwa na wahusika wanaowakilisha jamii kwani fasihi ni kioo cha jamii. Timothy Arege hajaachwa nyuma kuangazia suala la magonjwa kwenye kazi yake katika tamthilia za *Bembea ya Maisha na Mstahiki* Meya ambapo anajadili jinsi hali ya magonjwa inavyotishia kusitisha maisha ya wahusika wanaowakilisha binadamu katika jamii kwa vile fasihi ni kioo cha jamii. Madai haya ya magonjwa yanadhihirika kwenye sehemu zinazozungumziwa hapa;

Katika tamthila ya *Bembea ya Maisha*, ugonjwa unajitokeza pale ambapo Neema mtoto wa Sara na Yona anamwambia mama yake aliyekuwa na ugonjwa wa moyo uliosababishwa na mgogoro kati yake na mume wake. Ujumbe huu wa ugonjwa unadhihirika kwa mjadala kati ya Sara na bintiye Neema

> Kumbuka daktari alivyoshauri kuhusu ugonjwa wako uliosababishwa na mivutano kati yako na baba, mivutano hii imekusababishia ugonjwa wa moyo(uk46).

Vile vile, kwenye tamthilia ya *Mstahiki Meya*, inabainika kuwa pale kwenye zahanati ya Baraza la Cheneo kuna wagonjwa wengi wanaosaka matibabu huku wakiathiriwa na magonjwa tofauti. Madai haya yanajitokeza kwenye maneno ya Waridi katika dondoo hii ;
*‘‘ Lazima ufuate utaratibu. Wewe huoni urefu wa mstari huko nje ? au unafikiria kuwa hao wengine hawajakuja kutafuta matibabu ?’’* (uk 2)
Kauli ya kuwa kwa mstari mrefu ni ishara ku*wa* wagonjwa walikuwa wengi mno jambo ambalo linatishia ubora wa afya bora katika jamii.
Utafiti huu ulibaini kuwa jamii ya mwanadamu inakumbwa na changamoto za magonjwa ya kila aina ilhali uongozi wenyewe unashindwa na kukabiliana na hali hii nzito ya ongezeko la wagonjwa.

**Mauti**

Mauti ni hali ya kutokwa na uhai kwa kiumbe mwenye uhai yaani mwisho wa maisha ya mwilini. Hali ya kifo ni tata tangu mwanzo wa kuwepo kwa binadamu duniani na ni mojawapo ya masuala hatari yanayotisha mwanadamu katika kuishi kwake. Miaka ya hivi karibuni kumekuwa na vifo vya kiholelaholela vinavyosababishwa na makosa ya binadamu mwenyewe na vingine kutokea kwa sababu za hali ya kimaumbile isiyokuwa mikononi mwake. Kuongezeka kwa vifo duniani kumechochea jamii ya waandishi wa makala tofauti zikiwemo vitabu vya fasihi kuwa mstari wa mbele kuandika mada za vifo kwa lengo la kuhamasisha jamii kuhusu mbinu inayoweza kupambana na hali hii hatari maishani.

Waandishi wa tamthilia hawajaachwa nyuma kutumia wahusika kwa kazi zao ili kuwakilisha jamii ya kawaida inayoathiriwa na janga la mauti siku baada ya siku. Haya yanapatikana kwenye Tamthilia za *Bembea ya Maisha* na *Mstahiki Meya* za Timothy Arege ambapo watu wanakufa kwa magonjwa na ajali zinazoweza kuepukika jinsi inavyojitokeza kwenye kauli zifuatazo;

Katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*, kwenye mazungumzo kati ya Bunju na Neema, tunatambua kuwa Bunju ni yatima kwani wazazi wake wawili waliaga dunia. Vile vile kupitia mazungumzo ya wahusika hawa tunatambua kuwa Neema alipata ajali hapo awali ambapo watu wengi walipoteza maisha lakini Neema akanusurika. Hali ya mauti yanadhihirika kwenye maneno ya Neema katika dondoo hii; *‘‘Kwa bahati mbaya wazazi wako wametangulia mbele ya meza ya haki…. Baada ya ajali niliyokumbana nayo ilikuwa mbaya sana kwani roho nyingi zilipoteza uhai lakini mimi nikanusurika’’ (*uk 50-51)

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Daktari Siki anasema kuwa watu wengi wanakufa kwa njaa kwani hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi. Kauli ya Siki ipo kama ifuatavyo;

> Sikiza Meya Sosi, watu kadhaa wana shida na wengine wanakufa na njaa kwa sababu hawana uwezo wa kumudu mahitaji ya kimsingi na hivyo inahitajika uwasikize (uk 11).

Waridi anajuta mbele ya Daktari Siki kwa kudai kuwa alisikitika sana kuona mtoto wa mama akifia mikononi mwake pasipo na la kufanya. Haya yanadhihirika jinsi ilivyo hapa; *‘‘Nilisikitikia mtoto mdogo aliyefia mikononi mwangu bila lolote la kufanya ilhali naye mama mwenyewe anatarajia nimwokolee mwanawe’’ uk35).*

Naye kiongozi wa wafanyikazi Tatu anamwambia Siki kuwa anasikitika kwa kuona watu wakifa kwa kukosa dawa. Kauli ya Tatu inadhihirika kwa kauli hii *‘‘Nasikitika sana kwa kuona watu wakifa kwa sababu ya kukosa dawa badala ya labda wangekufa kwa kushindwa kuzilipia ingekuwa afadhali’’(uk38*)

Utafiti huu ulibaini ukweli ulio wazi kuwa jamii inakumbwa na mauti ambayo yanaweza kuepukika iwapo jamii yenyewe itawajibika kuziba mianya inayoleta yale mauti.

**Ongezeko la Uchafuzi wa Mazingira**

Uchafunzi wa mazingira ni hali ya kuharibu mambo yote yanayomzunguka kiumbe katika maisha yake. Mazingira yanapochafuliwa, hali ya hewa huharibika na hivyo kuathiri viumbe waliozungukwa na mazingira husika. Harufu huwa mbaya na wakati mwingi hutaabisha walio karibu na kuwakosesha amani ya moyo.

Mara nyingine uchafuzi wa mazingira huweza kuzua magonjwa kwa viumbe walio karibu na haswa binadamu. Kwa vile fasihi na mwanadamu huwa kitu kimoja kisichotenganishwa, waandishi tofauti wamekuwa wakiangazia suala la uchafunzi wa mazingira kwa lengo la kuhamasisha umma na sekta zote zinazohusiana na mazingira. Masuala haya yameangaziwa na Timothy Arege katika tamthilia zake za *Bembea ya Maisha* na *Mstahiki Meya* ambapo anajadili namna uongozi mbaya unavyochangia ongezeko la uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha hali za kiafya za wananchi. Haya yanajitokeza kwenye kauli zilizo kwenye mijadala ifuatayo;

Katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*, mhusika Asna analalamikia harufu mbaya iliyopo kwenye wodi za hospitali za nyumbani. Hili linadhirisha kuwa ukosefu wa unadhifu umefanya mazingira kuwa machafu kule kiasi cha kukosesha wagonjwa matumaini ya kuishi jinsi ilivyo hapa chini *‘‘Kuna harufu mbaya pale hosipitalini inayotokana na dawa kwenye wodi za wagonjwa’’ uk42*)

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Gedi anamwambia Meya kuwa harufu aliyohisi haikutokana na maji aliyompa bali ilitokana na taka iliyojaa barabarani.
“*Hiyo harufu haitokani na maji niliyokupa sir bali inatokana na harufu ya taka barabarani na ambayo imefika humu baada ya mkondo wa upepo kubadilika na kuelekea humu’’(uk19*),
Waridi naye anamwambia Siki kuwa atajiuzulu kazi kwani mazingira ya hospitalini wanamofanyia kazi pametawaliwa na nzi na kuhatarisha hali yao pale kama inavyodhihirika hapa;
‘‘*Hii hospitali ni chafu na hakuna maji ya kutosha. Pia nzi wametawala usafi na hivyo kuhatarisha hali yetu ya kuwepo hapa’’(uk36*).
Kisha kiongozi wa wafanyikazi Tatu anamfahamisha Meya kuwa mji wa Cheneo umejaa uvundo kiasi cha kuzuia wageni kufika pale, majitaka yaliyopo pia yanatishia kuleta ugonjwa wa kipindupindu wakati wowote. Kauli hii ya Tatu inadhihirika kwenye dondoo ifuatayo;
‘‘*Sikiza Meya, uvundo uliopo jijini utawazuia wageni kuingia humu, vyoo ni vichafu na majitaka yamezagaa kote. Ugonjwa wa kipindupindu unaweza kuzuka wakati wowote’’ (uk 72*)
Kulingana na utafiti uliofanywa ni wazi kuwa kuna changamoto ya ongezeko la uchafuzi wa mazingira suala ambalo ni hatari kwa afya za wanajamii wenyewe.

**Wizi**

Wizi ni kitendo cha kuchukua kitu cha wengine bila idhini yao. Mara nyingi wezi hutekeleza vitendo vya wizi pasipo na kuonekana au kwa siri wasije wakaonekana na wenyeji. Kwa sababu ya mmomonyoko wa maadili unaozidi kukithiri miongoni mwa wanajamii siku baada ya siku, wizi unazidi kushuhudiwa kwa kiasi kikubwa katika mazingira ya mwanadamu.

Wizi unaathiri jamii moja kwa moja kwani inabidi mazingira yaliyo na wizi yalindwe kwa vyovyote vile ili wizi usitokee. Fasihi ni mojawapo ya vitengo vinayosawiri masuala nyeti katika jamii na hivyo basi waandishi wa vitabu vya fasihi wameangazia suala la

changamoto za wizi linalozidi kupanuka siku baada ya siku. Maudhui ya wizi yameangaziwa kwenye riwaya, hadithi fupi na tamthilia. Mojawapo ya tamthilia ambazo wizi umeangaziwa ni zile za Timothy Arege za Bembea ya Maisha na Mstahiki Meya namna ilivyo kwenye kauli zifuatazo;

Katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*, kuna mazungumzo kati ya Yona na bintiye Neema ambapo Yona anamwambia bintiye kuwa hata kama anawapa wafanyikazi vibarua kule shambani, inabidi yeye mwenyewe awepo ili wasimwibie. Kauli ya Yona inajitokeza kwenye dondoo ifuatayo;

> Kazi za shamba zinakungoja, kwani hata ukiwapa watu kibarua inabidi uwe pale uwalinde siku nzima la sivyo utapata wamekupunguzia kile kidogo walichokuja kukutengenezea (uk72).

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Bili anawashauri Meya Sosi, Diwani I na Diwani II wapange mikakati ya kuiba fimbo ya meya kwani ni dhahabu tupu kisha watangaze kuwa iliibiwa wakati wa maadamano. Kauli ya Bili imo kwa madondoo yafuatayo;

> Fimbo ya Meya ipo...Utabeba dhahabu mkononi kwani ni tope? ...Ni nani atadhubutu kukangua Bwana Usalama hapa? ...Baada ya wiki tatu Bwana Usalama arudi hapa atangaze kuwa fimbo imeibiwa wakati wa rabsha iliyotokea…Wakati huo fimbo itakuwa tayari imeuzwa ng'ambo (uk62).

Utafiti uliofanywa ulibaini kuwa wizi umekuwa changamoto kuu katika jamii. La kushtua Zaidi ni kuwa wizi huu pia unaendelezwa na viongozi wanaotarajiwa kuwa kielelezo bora kwenye jamii inayoibuka na uozo wa kila aina siku baada ya siku.

**Mizozo ya Ndoa**

Ndoa ni makubaliano rasmi ya watu wawili haswa wa jinsia ya kiume na kike kuishi pamoja kama mume na mke. Makubaliano haya hulenga kuwa ya daima hadi watenganishwe na kifo au masuala yasiyoweza kuepukika. Hata hivyo, kuna mivutano mingi kwenye ndoa inayotishia kukatisha makubaliano haya pasipo na muamano.

Hii imekuwa changamoto kubwa na haswa kwenye jamii ya karne ya ishirini na moja. Kuna viini kadhaa vinavyochangia mizozo hii vikiwemo mipango ya kando, hali ya kiuchumi, utengano wa muda mrefu na utasa miongoni mwa viini vingine. Mizozo katika ndoa imekuwa ikiangaziwa katika fasihi ya vitengo vyote kwani fasihi hutumika na jamii kama kielekezo cha maisha yao.

Timothy Arege anaangazia mzozo wa ndoa katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*, mzozo uliomo kati ya Bunju na mkewe Neema. Haya yanadhihirika kwenye kauli zifuatazo;

> Wewe huelewi, siwezi kuacha kwenda kuvuta riziki niende michezoni…Nimekupa uhuru lakini uhuru huo unaanza kukulevya. Umeunda serikali yako ndani ya nyumba yangu…Umesahau kuwa mimi ndiye mume na kichwa cha nyumba hii na wewe ni shingo. Naona ushakata ubeleko na unachosubiri tu ni siku ya siku (uk48-49).

Utafiti huu ulibaini kuwa kuna changamoto kuu kwa jamii kwenye ndoa za watu wake. Mizozo hii inakosesha amani nyumbani kiasi cha kusabaratisha ndoa zenyewe.

***Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: ISSN 2523-6725 (online)**
**October 2024 Vol. 8, No. 10**
**Citation:** Kimwe, P & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Za Maisha Katika Tamthilia Za Kiswahili: Uchunguzi Wa *Bembea Ya Maisha* Na *Mstahiki Meya*. *Journal of African Interdisciplinary Studies*, 8(10), 199 – 214.

**Unafiki wa Kidini**

Unafiki ni hali ya mtu kujifanya kuwa mwema au asiye na doa mbele ya watu ilhali anajificha na kutenda yaliyo kinyume na matarajio. Unafiki wa kidini ni hali ya mtu kujifanya kuwa ni mcha mungu mbele ya watu ilhali anatenda kinyume na mafundisho ya mungu huyo akiwa amejificha. Katika jamii ya mwanadamu, wanadini hutarajiwa kuwa kielelezo kwenye jamii inayozidi kuoza kila uchao.

Hata hivyo, miaka ya hivi karibuni wanadini wamejawa na uovu usiotarajiwa na kuwa sawa tu na wasioamini au hata kuwa waovu Zaidi. Hii imekuwa changamoto kuu katika jamii kwani vielelezo vya kuigwa vinazidi kupungua kila uchao. Kwa vile fasihi ni kioo cha jamii ya mwanadamu, wanafasihi wamekuwa mstari wa kwanza kuangazia changamoto hii ili kujaribu kukemea unafiki huu angalau kujaribu kurudisha jamii kwenye mwangaza uliotarajiwa na waanzilishi wa dini. Timothy Arege anaangazia unafiki wa kidini kwenye tamthilia za *Bembea ya Maisha* na Mstahiki Meya mtawalia.

Kwenye tamthilia ya *Bembea ya Maisha*, Arege anaangazia Yona na wenzake waliokuwa wanadini kamili wakiwa chuo kikuu ila walishiriki ulevi wakiwa wamejificha. Ulevi ni kinyume na mafundisho ya dini na haswa kwa wanaodai kuwa ‘wameokoka’. Hayo yanajitokeza kwenye kauli ifuatayo ya mazungumzo ya Yona na Beni;

*‘‘Wenzenu ndio walioniingiza kwenye mkondo wa ulevi. Kumbuka nilikuwa miongoni mwa vijana wa kwanza kuingia kwenye dini. Hata tulikuwa wahubiri’’*

Kwenye tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Arege anaangazia unafiki unaoendelezwa na mhubiri anapoenda kumwombea mstahiki meya ofisini mwake kwa malipo ya sadaka nono huku akijua fika kuwa Meya anaendeleza maovu ya kudhulumu raia kwenye Baraza la Cheneo. Mafundisho ya kidini yanampasa Mhubiri kumshauri abadilishe mienendo yake. Unafiki huu unajitokeza kwenye kauli hizi kati ya Meya na Mhubiri na pia kati ya *Meya na Bili* jinsi ilivyo hapa;

> Hata Mhubiri yuko nyuma yako, nimekutana naye na akanihakikishia hivyo. Akikuweka mikononi mwa Bwana hakuna litakalokushinda…Nitamwambia unahitaji maombi yake’ ’( uk33)… ‘‘Ni furaha yangu kuona wanasiasa kama wewe wakiutafuta upendo wa Bwana..Uongozi unaotafuta dini utadumu maana umebarikiwa (uk41).

Utafiti huu ulibaini kuwa badala ya wanadani kuwa kielelezo mwafaka cha kuangazia jamii, wamejawa na unafiki jambo ambalo limekuwa changamoto kwa jamii ya mwanadamu kwani inazidi kudindimia kimaadili siku baada ya siku.

**Kodi za Juu**

Kodi ni malipo yanayofanyika kutokana na mkataba ambao umeanzishwa na uongozi wowote wa jamii na haswa serikali. Kwa jamii zilizostawi, kodi hutumika kwa kujenga miundo msingi kwenye sekta tofauti za nchi yao. Kodi kwa mara nyingi huandamana na mapato ya nchi na iwapo mapato yako juu basi kodi huwa juu na iwapo kiwango cha mapato kipo chini basi nayo kodi hupungua pia. Lakini kwa sababu ya uongozi wa binadamu kujawa na ufisadi na tamaa, hali imekuwa tofauti sana na mara nyingi jamii iliyodhulumika kimapato hujipata kulipa kodi ya juu hali ambayo hukatisha tamaa kwa waathiriwa.

Kutia msumari moto kwenye kidonda kibichi ni kuwa hata ile kodi raia wa kawaida wanalipa haiwafaidi kamwe ila hufisidiwa na viongozi wao. Jamii ya waandishi imekuwa

*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: **ISSN 2523-6725** (online)
**October 2024 Vol. 8, No. 10**
**Citation:** Kimwe, P & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Za Maisha Katika Tamthilia Za Kiswahili: Uchunguzi Wa *Bembea Ya Maisha* Na *Mstahiki Meya*. *Journal of African Interdisciplinary Studies*, 8(10), 199 – 214.

kwenye msitari wa kwanza kuandika kuhusu masuala ya kodi ili kuleta mwanga kwa jamii iliyosoma kuelewa faida na hasara zinazoweza kushuhudiwa iwapo suala la kodi litadhihakiwa.

Suala la kodi limejadiliwa na Timothy Arege kwenye vitabu vyake vya *Bembea ya Maisha* na *Mstahiki Meya* ambapo raia wa kawaida wanazidi kuumizwa na serikali zao kwa kutozwa kodi ya juu isiyowafaidi bali hufisidiwa na uongozi uliopo. Vile vile, kinachowaumiza raia zaidi ni kuwa uongozi unaamua kuwa viongozi hawapaswi kulipa kodi kwani wanatumikia raia. Kitendo hiki kinadhihirisha namna uongozi mwingi wa jamii ya leo unavyoweka maslahi yao mbele pasipo kujali wanaoongozwa na hili linazidi kuzua uhasama kati ya uongozi na wananchi wa kawaida. Changamoto hii ya kodi ya juu inadhihirika kwenye kauli zilizojadiliwa hapa chini;

Katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*, Asna anamwambia mama yake Sara kuwa chumba anamoishi hulipiwa kodi ya juu inayolingana na vyumba viwili katika mitaa mingine na hivyo basi sio kila mtu anayeweza kuishi kwenye mtaa anamoishi Asna. Udhibitisho wa kauli ya Asna unatokea hapa chini;

*‘‘Sio kila mtu anayeweza kuishi kwenye mtaa huu kwani ingawa chumba wakiona kidogo, kodi yake ni mara dufu katika mitaa nyingine’’(uk31*)

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Diwani III analalama kuwa wanyonge wanatozwa kodi ya juu ili kugharamia starehe za viongozi huku viongozi wenyewe wakipunguziwa mzigo wa kulipa kodi yenyewe hali ambayo inazidi kuumiza mnyonge huyu. Kauli ya Diwani III yanadhihirika katika dondoo hii;

*Mama muuza ndizi amepandishiwa kodi ili kusaidia kujenga taifa itakuwaje sisi madiwani tukose kulipa kodi?’’*uk22)

Utafiti huu ulibaini kuwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na changamoto za kodi za juu suala ambalo limefanya wengi wa wanajamii kukabwa koo na kodi hizi na hivyo basi kukatizwa tamaa na maisha yenyewe.

**Ukosefu wa Huduma za Kimsingi**

Huduma za kimsingi ni shughuli zozote zinazoweza kufanywa na mtu kwa manufaa ya mwingine ili kufanya hali ya mtu huyo kuwa tulivu na yenye amani. Ni vigumu kwa binadamu kuishi bila huduma hizi kwani zinamshkilia kusukuma maisha yake ya kila siku. Baadhi ya huduma hizo ni zile za afya bora, maji safi, chakula safi na salama, mavazi bora, makazi bora miongoni mwa zingine. Kwa vile huduma hizi za kimsingi zinaungana moja kwa moja na jamii ya mwandamu, waandishi wengi na haswa wa fasihi wamekuwa kwenye msitari wa kwanza kujadili hali hii kwenye kazi zao ili kuhamasisha umma kuhusu hali zinazowakabili. Mijadala hii ya ukosefu wa huduma za kimsingi inapatikana kwa vitabu vya fasihi vikiwemo vile vya tamthilia za Timothy Arege za *Bembea ya Maisha* na *Mstahiki Meya* mtawalia jinsi inavyojitokeza hapa chini.

Katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*, kwenye mazungumzo kati ya Sara na mwanawe Asna, tunatambua kuwa kwenye hospitali za nyumbani kuna huduma duni. Wahudumu hawana mhalaka mwema, wodi zimejaa harufu ya dawa kote navyo vitanda havina shiti. Hali hii inakosesha mgonjwa matumaini ya kuishi kama anavyosema Asna kwenye dondoo ifuatayo ;

*‘‘Ukilazwa kule ni kama umeingia seli, kisa na maana wahudumu wamejawa na vitisho na amri kama askari, harufu ya dawa imeenea kote na hamna shiti vitandani. Hali nzima pale inakukosesha mgonjwa matumaini ya kuwa bora kwa afya yake*’’(*uk42*.)

*Journal of African Interdisciplinary Studies (JAIS)*: **ISSN 2523-6725** (online)
**October 2024 Vol. 8, No. 10**
**Citation:** Kimwe, P & Gakuo, J. K. (2024). Usawiri Wa Changamoto Za Maisha Katika Tamthilia Za Kiswahili: Uchunguzi Wa *Bembea Ya Maisha* Na *Mstahiki Meya*. *Journal of African Interdisciplinary Studies*, 8(10), 199 – 214.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Daktari Siki amamfahamisha Meya Sosi kuwa huduma za matibabu haziko kwani hakuna dawa kwenye zahanati (uk11). Diwani III anakashifu Diwani I, Diwani II na Meya kwa kuwahadaa kuwa dawa zipo njiani ilhali hakuna aliyeziagiza. Kauli ya Diwani III ipo kwenye kauli ifuatayo ;
*''Watu wana njaa na hawana dawa licha ya kuwa tunawahadaa zipo njiani ilhali hamna aliyeziangiza'' (*uk21)

Kulingana na utafiti huu ni dhahiri shahiri kuwa jamii ya mwanadamu inakumbwa na changaamoto kubwa ya ukosefu wa huduma za kimsingi. Kwa vile huduma hizi ni muhali kwa maisha ya kila siku, inabidi binadamu kutaabika pasipo na la kufanya baada ya kupuuzwa na viongozi waliojukumizwa kukabiliana na hali hii.

**Mfumuko wa Bei za Bidhaa**

Mfumuko wa bei ni hali ya kupanda kwa bei ghali na ambayo hupanda kwa haraka bila ya kutarajia na pasipo na mpango baada ya kushuka kwa thamani ya fedha. Mfumuko huu unapotokea huathiri jamii na haswa wale wa tabaka la chini na lile la kati na kupunguza maendeleo ambayo wangefanya kwani hela nyingi hutumika kugharamia maisha ya mfumuko huu. Mara nyingi mfumuko huu huletwa na uongozi mbaya na haswa ulio fisadi kwani viongozi hutumia mali ya umma visivyo kwa masuala yao ya kibinafsi.

Wakati mwingine viongozi hukopa fedha kutoka mataifa ya nje na badala ya kuwekeza kwenye sekta zitakazoleta faida kwa taifa, viongozi hawa hufisidi hela hizi kwa matumizi yao ya kibinafsi. Kwa vile mfumuko wa bei huathiri jamii moja kwa moja, waamdishi wa kazi za fasihi wamekuwa msitari wa mbele kuandika kuhusu hali hii.

Kazi za mfumuko wa bei zimejadiliwa kwenye tamthilia za Kiswahili zikiwemo zile za *Bembea* ya *Maisha na Mstahiki Meya* za Timothy Arege. Mfumuko huu umeathiri wanajamii kiasi cha kulilia serikali zao ili ziwashughulikie kuwashusha mzigo mzito kwao. Changamoto ya mfumuko wa bei unadhihirika kwenye tamthilia teule jinsi ifuatayo;

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mfumuko wa bei unajitokeza katika mazungumzo kati ya muuguzi Waridi na mama aliyeleta mtoto mgonjwa. Mama huyu anadai kuwa hakuweza kutokosa maharangwe yaliyolala kabla ya kumpa mtoto wake kwani bei ya makaa na ile ya mafuta zimepanda kwa kiasi kikubwa ambacho mtu wa tabaka la chini hawezi kuimudu. Kauli ya madai haya yamo kwenye dondoo hii ya maneno ya Mama kwa Waridi ;
'*'Moto tutatoa wapi mwanangu, bei ya makaa ya imepanda baada ya sheria ya misitu kupitishwa nayo bei ya mafuta taa inapanda siku baada ya siku''* (*uk 5*)

Vile vile katika mazungumzo kati ya Daktari Siki na kiongozi wa wafanyikazi Tatu, ni kuwa Tatu anasema kuwa bei ya dawa imekuwa ghali mno kiasi cha wafanyikazi kutoimudu kwani malipo yao ni duni.
Utafiti huu ulibaini peupe kuwa jamii inakabiliana na changamoto kuu ya mfumuko wa bei suala ambalo linaifanya jamii yenyewe kuwa na maisha magumu ya kukabiliana na hali ngumu ya kiuchumi.

**Hitimisho**

Kulingana na utafiti huu, jamii imejawa na wingi wa changamoto ambazo zinawaathiri watu wake moja kwa moja. Changamoto hizi husababishwa na binadamu mwenyewe na zingine ni za kimaumbile na hazimo mikononi mwake. Yaliyoangaziwa yanadhihirisha wazi kuwa japo dunia ya mwanadamu imejawa na changamoto za kila aina, binadamu huyu ndiye tu anayepaswa kuwa mstari wa kwanza kukabiliana na yanayomkabili. Hii ni kwa sababu ingawa maisha hukumbwa na baadhi ya changamoto za kimaumbile ambazo hazimo

mikononi mwa binadamu, asilimia kubwa ya changamoto hizi huzaliwa kwenye mazingira anamoishi binadamu huyu na kuwa yeye ndiye chanzo kikuu cha yanayomkabili siku baada ya siku. Utafiti huu umeng'amua pakubwa kuwa binadamu asipojiathari na kusaka jinsi atakavyopunguza changamoto hizi za maisha basi zitazidi kumkatisha tamaa siku baada ya siku kwani hata akijiachilia kwa jaala itazidi kumhukumu bila huruma. Kwa vile Muumba amemtunukia binadamu akili razini, binadamu huyu hana budi kujizatiti kujitengenezea dunia ya kesho iliyo na afadhali kuliko ya leo isije ikadhulumu vizazi vyake vitavyozuka baada yake.

## Marejeleo

Arege, Timothy, M. (2009). *Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.
Arege, Timothy, M. (2021). *Bembea ya Maisha*. Nairobi: Access Publishers Limited.
TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahil Sanifu*. Dar es salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
Wafula, R na Njogu, K. (2007): Nadharia za uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
Wafula, R. (1999): 'Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake.' Nairobi: Jomo Kenyatta Foundations.
Wamitila, K (2008): Kazi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Nairobi: Vide-Muwa Publishers
Wamitila, K. (2002). Uhakiki wa Fasihi: misingi na vipengele vyake. Nairobi: Focus Publication.
Wamitila, K. (2003) Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia. Nairobi: Focus Books.
Wamitila, K. (2003), Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi. English press: Nairobi